# MWONGOZO WA MWELIMISHAJI WA MWONGOZO WA SOMA NYUMBANI:

Taarifa zifuatazo zinawalenga waelimishaji. Unapochapa mwaongozo huu kwa ajili ya familia, tafadhali jumuisha Mwongozo wa Familia wa Soma Nyumbani (Kurasa 2-21

Lengo la Mwongozo wa Familia wa Soma Nyumbani ni kuwasaidia waalimu katika kuziwezesha na kuzitia moyo familia pale zinapotumia Mpango wa Mtoto wa Soma Nyumbani. Mwongozo huu unatoa taarifa ili kuimarisha uelewa wao kuhusu kile ambacho watoto wanapaswa kukijua na kuweza kukifanya kwa ajili ya usomaji wenye stadi, na pia shughuli za kuwasaidia watoto wao wawe wasomaji wenye ustadi. Ili kulifikia hili, Mwongozo wa Familia wa Soma Nyumbani unajumuisha:

1. Matokeo ya kipimo na uchunguzi ya ulimwengu mzima inayojazwa na mfanyakazi wa shule
2. Uteuzi wa maeneo ya usomaji ambayo watoto wao wanahitaji msaada zaidi kuyaendeleza, na
3. Uzoefu wa ujifunzaji wanaoweza kuufanya nyumbani na watoto wao ili kuwezesha ukuzaji wa stadi za usomaji.

Kurasa za utangulizi zinazofuata hujumuisha barua ya taarifa kwa familia pamoja na fomu ili wasilisha data za upimaji wa mwanafunzi, na maeneo ya usomaji ambayo mtoto yuko kwenye hatari ya kutoweza kuifikia kiwango.

Halafu, mwogozo huo unatoa muktadha kwa kutoa taarifa za wazazi kuhusu:

- Sheria ya Soma Ufanikiwe iliyoanzishwa katika Muswada wa Seneta 9 (2022);
- Mpango wa Uboreshaji wa Usomaji;
- Mpango wa Soma Nyumbani na;
- Faharasa ya istilahi za kusoma kwa usaidizi wa ziada.

Kurasa za mwisho zitaonekana kuwa za msaada zaidi kwa kuwa zimepangwa katika vijenzi vitano muhimu vya usomaji (utambuzi wa kifonimu, elimu ya sauti, utiririfu, msamiati na ufahamu). Sehemu hiyo inajumuisha:

- Maelezo rafiki ya familia kuhusu vijenzi vya usomaji: na
- Uzoefu wa kusoma nyumbani ili kuhimiza na kuwezesha maendeleo ya usomaji wa darasani.

Shughuli zilizotolewa katika Mpango wa Soma Nyumbani hauhitaji maandalizi yoyote ya mwalimu. Hata hivyo, mapitio ya haraka haraka ya shughuli hizo pamoja na mapendekezo ya seti za herufi na maneno yatasaidia kuhakikisha kwamba wanafunzi hawatakiwi kujiingiza katika ujifunzaji mpya nyumbani. Waelimishaji lazimwa wapendekeze shughuli kwa ajili ya wanafunzi kulingana na mahitaji yao.

Kurudufu na kuushirikisha Mwongozo wa Familia wa Soma Nyumbani kwa familia za wanafunzi ambao wapo katika hatari ya kutofikia viwango unahimizwa. Waalimu wanaweza kuamua kupeleka nyumbani kwa mwanafunzi aliye hatarini sehemu za utangulizi pamoja na sehemu tano za shughuli, au sehemu ya utangulizi na sehemu ya shughuli moja au zaidi kwa mara moja. Vyovyote iwavyo, umakini wa mwalimu unapendekezwa.

# MWONGOZO WA FAMILIA WA MPANGAO WASOMA NYUMBANI

**Wapendwa Wazazi na Waangalizi,**

Wasimamili na waelimishaji wa JCPS wa ______________ wanathamini wajibu wenu na kutambua mchango mlionao kwa maendeleo ya kielimu ya watoto wenu. Tunathamini ushirikiano imara kati ya shule na familia, na tunatambua kwamba ushirikiano imara hujengwa katika mawasiliano na usaidizi wa dhahiri. Mwongozo huu wa Mpango wa Familia wa Soma Nyumbani umeundwa katika maadili haya na unasaidia Mpango wa Uboreshaji wa Usomaji wa mtoto wako. Kurasa zifuatazo zinajumuisha maelezo taarifa kuhusu:

1. Matokeo ya mtoto wako ya kipimo na uchunguzi wa kiulimwengu;
2. Maeneo ya usomaji ambayo mtoto wako anahitaji usaidizi zaidi kuyakuza; na
3. Uzoefu wa ujifunzaji unaoweza kuufanya nyumbani na mwanao ili kuwezesha ukuzaji wa stadi za usomaji.

Zaidi ya hayo, kuna taarifa kuhusu Sheria ya Kentucky ya Soma Ufanikiwe kulingana na Muswada wa Seneta 9 (2022), Mpango wa Kuboresha Usomaji, Mpango wa Soma Nyumbani pamoja na majukumu ya msingi ambayo familia zinafanya katika mafanikio ya mwanafunzi. Faharasa za istilahi za kusoma na vidokezo vya jumla kwa kusoma nyumbani vimejumuishwa pia.

Uzoefu wa ujifunzaji wa nyumbani uliojumuishwa katika waraka huu umepangiliwa katika vijenzi vitano vya msingi vya usomaji (utambuzi wa kifonimiki, elimu ya sauti, utiririfu, msamiati na ufahamu). Mara utakapojua maeneo ambamo mtoto wako anahitaji msaada zaidi, utawezeshwa kuzingatima muda wako katika shughuli zilizojumuishwa kwenye ile sehemu ya mpango huu. Kutumia muda katika uzoefu wa ujifunzaji katika sehemu nyingine una himizwa pia, kwani usomaji stadi hutegemea kuwa na mafanikio katika maeneo hayo yote matano.

Idare ya Elimu ya Kentucky inayofuraha kushirikiana na viongozi pamoja na walimu wa shule ya mtoto wako ili kutoa msaada kupitia Mpango huu wa Soma Nyumbani. Kama una swahli kuhusu taarifa au ujifunzaji uliopendekezwa katika mpango huu, tafadhali wasiliana na mwalimu wa mtoto wako

**Wako,**
**Mkuu wa Chuo**

# MWONGOZO WA FAMILIA WA MPANGAO WASOMA NYUMBANI

## TAARIFA YA TATHMINI YA KIPIMO NA KIUCHUNGUZI WA KIULIMWENGU.

**(Ijazwe na mwelimishaji)**

| | |
|---|---|
| Jina la Mwanafunzi | |
| Darasa | |
| Jina la Mwalimu | |
| Tarehe | |
| Maeneo ya Uboreshaji wa Usomaji<br><br>Mkakati Uliopo | |
| Imejazwa Na | |

### TAARIFA YA MATOKEO YA TATHMINI YA KIPIMO NA KIUCHUNGUZI YA KIULIMWENGU

| Jina la Tathmini | Aina ya Tathmini | Mwanzo wa Mwaka Alama/Kiwango | Katikati ya Mwaka Alama/Kiwango | Mwisho wa Mwaka Alama/Kiwango |
|---|---|---|---|---|
| Ukuaji wa MAP | **Kipimo** | | | |
| Utiririfu wa Usomaji wa MAP | **Uchunguzi** | | | |
| | | | | |
| | | | | |

### ENEO LA UZINGATIVU KWA KUTOKUFIKIA MALENGO YA NGAZI YA DARASA

**(Chagua yote yanayofaa kulingana na UTIRIRIFU WA USOMAJI WA MAP. Ambatisha data.):**

○ Utambuzi wa Kifonimiki
○ Elimu ya sauti
○ Utiririfu
○ Msamiati
○ Ufahamu

# MWONGOZO WA FAMILIA WA MPANGAO WASOMA NYUMBANI

## MAANA YA MPANGO WA UBORESHAJI WA USOMAJI NA JINSI FAMILIA ZINAVYOWEZA KUSAIDIA

Sheria ya Soma Ufanikiwe ilisainiwa kuwa sheria mwaka 2022. Mwanafunzi yeyote katika shule ya awali mpaka daraja la tatu ambaye anajulikana kama mwenye uhitaji wa ujifunzaji wa msukumu ili asonge kuelekea kwenye ustadi wa kiutendaji katika kusoma atapewa **Mpango wa Ukuzaji wa Usomaji** ulioandaliwa na kufanyiwa kazi na **Timu ya Ukuzaji wa Usomaji**.

Timu ya Ukuzaji wa Usomaji huandaa na kusimamia mchakato wa mpango wa ukuzaji wa usomaji na hujumuisha:

- Mzazi au mlezi wa mtoto anayehusika na mpango wa kukuza usomaji;
- Mwalimu mmoja wa wa elimu wa kawaida wa mtoto wa kutoa taarifa kuhusu mtaala wa jumla wa wenziwe wa mtoto wenye rika moja;
- Mwakilishi wa wakala wa elimu wa eneo husika ambaye anaujuzi juu ya mtaala na upatikanaji wenye ushahidi wa rasilimali za usomaji za wakala wa ndani; na
- Waajiliwa wowote washule wabobezi waliothibitishwa kwa ajili ya watoto wanaopokea maelekezo ya lugha, upangaji wa kielimu au huduma za elimu maalum.

Huku mzazi au mlezi wa mwanafunzi husika wa mpango akiwa mwanachama wa timu hiyo, familia na waangalizi wengine pia wanaweza kumsaidia mwanafunzi kwa kuurejea mwongozo huu kwa taarifa juu ya namna mtoto anavyojifunza kusoma na kumpa uzoefu mzuri wa kujifunza ili kumsaidia mtoto katika kukuza stadi zake nyumbani.

**Mpango wa Kukuza Usomaji** lazima ujumuishe taarifa kuhusu kiwango cha sasa cha mafanikio cha mtoto wako katika usomaji, maeneo ambamo anaweza kufanya maboresho ya kina na maelezo ya usaidizi na huduma za msaada ambazo zitatolewa kwa mtoto wako. Usaidizi lazima ujumuishe mikakati ya kiuelekezaji na rasilimali za kufaa za kiuelekezaji zinazotakiwa ili kumsaidia mtoto aonyeshe maendeleo ya haraka. Data za maendeleo ya mtoto wako pia zitajumuishwa katika mpango na zitatolewa kwa mzazi au mlezi kwa robo mwaka na zinaweza kujumuishwa kwenye kadi iliyoto ya ripoti ya mtoto. Maendeleo yataitaarifu timu ya ukuzaji wa usomaji kuhusu mafanikio ya usaidizi na itawaruhusu kufanya maamuzi ya kimaelekezo ili kumsaidia mtoto wako katika kusonga mbele kwenye usomaji mahiri.

**Mpango huu wa Soma Nyumbani** unatolewa kwa wazazi na walezi wa kisheria wa mtoto aliyetambuliwa kwa ajili ya usaidizi katika usomaji. Mpango huu unajumuisha taarifa za namna ya kushiriki katika shughuli zinazoongozwa na mzazi za usomaji nyumbani. Viwango vya Kielimu Vya Kentucky Njia Mpya ya Kuendelea ni rasilimali nyingine inayopatikana kwa familia.

# MWONGOZO WA FAMILIA WA MPANGAO WASOMA NYUMBANI

## FAHARASA YA ISTILAHI ZA KUSOMA

Vijenzi 5 vya Muhimu vya Usomaji: Haya ni maeneo yaliyounganishwa ya ujifunzaji yanayowezesha ustadi wa usomaji.

1. UTAMBUZI WA KIFONIMIKI

   Uwezo wa kutofautisha, kuzalisha, kukumbuka na kubaini sauti moja moja (fonimu) katika maneno yanayotamkwa.

2. ELIMU YA SAUTI

   Ujuzi wa uhusiano unaotabirika kati ya fonimu na miambatano (miunganiko ya herufi inayowasilisha fonimu) na uhusiano kati ya mafungu makubwa ya herufi na silabi au sehemu za maneno zenye maana (mofimu).

3. UTIRIRIFU

   Uwezo wa kusoma matini kwa kasi na usahihi wa kutosha ili kuwezesha ufahamu.

4. MSAMIATI

   Ujuzi wa maana ya neno moja moja katika matini na dhana ambazo maneno hayo yanabeba.

5. UFAHAMU

   Mchakato tata wa kuelewa na kutumia matini kwa njia ya kung'amua ujuzi wa awali na kujadili kwa mdomo, ambayo yote yanatumiwa na wasomaji wazuri kuelewa, kukumbuka na kuwasilisha kile kimesomwa.

### Hatarini kwa kutofikia malengo ya hatua za kidarasa:

Kuwa na maeneo mahsusi ya ukuaji katika eneo moja au zaidi la vijenzi vya usomaji kama vilivyotambuliwa na data za tathmini za kipimo na uchunguzi wa kiulimwengu. Wanafunzi wanaotambuliwa watahitaji usaidizi wa kimsaada kupitia Mpango wa Kukuza Usomaji ili kuonyesha mahitaji ya ujifunzaji unaoharakishwa katika usomaji.

### Usaidizi:

Kwa nyongeza, makundi madogo mahsusi au maelekezo ya mtu mmoja ili kuongeza au kukuza stadi katika vile vijenzi vitano vya usomaji (utambuzi wa kifonimu, elimu ya sauti, utiririfu, msamiati, na/au ufahamu)

### Programu za ustawishaji:

Usaidizi unaoharakishwa ndani au nje ya siku au kalenda ya shule unaoongozwa na watu wenye vigezo ili kutoa usaidizi ambao unajumuisha upangaji wa kimaelekezo wa usomaji wenye ushahidi unaohusiana na mikakati ya kimaelekezo yanayoelekezwa kwenye vigezo vya kuandika na kusoma vinavyotakiwa na KRS 158.6453 na kuelezewa kanuni za kiusimamizi zinazotolewa na Bodi ya Elimu ya Kentucky.

### Uangalizi wa maendeleo:

Upimaji endelevu wa mara kwa mara wa maendeleo ya mtoto kuelekea malengo ya usaidizi.

### Tathmini ya kiuchunguzi ya usomaji:

Tathmini ambayo hupima stadi za mwanafunzi dhidi ya hatua zilizowekwa za utendaji katika vijenzi muhimu vya usomaji, na huwatambua wanafunzi ambao wanahitaji usaidizi angalau katika moja ya vijenzi hivyo ili kuharakisha maendeleo ya mtoto kuelekea utendaji mzuri katika usomaji.

### Kipimo cha kiulimwengu:

Mchakato wa kutoa tathmini fupi kwa wanafunzi wote katika ngazi ya darasa fulani ili kutathmini utendaji wa watoto katika vijenzi muhimu vya usomaji.

# MWONGOZO WA FAMILIA WA MPANGAO WASOMA NYUMBANI

**VIDOKEZO VYA JUMLA KWA KUSOMA NYUMBANI**

- Ongeza muda wa kusoma siku nzima, na ufanye vitabu vipatikane nyumbani, kwenye begi la mgongoni au gari. Kusoma na mtoto wako kwa dakika 20 kunaweza kuwa na matokeo chanya ya kudumu.



- Pitisha kidole chako juu ya maneno unapoyasoma.
- Msahihishe mtoto wako kwa upole anapolisoma neno vibaya, hata kama yanakaribiana na yana maana sawa. Mfano, mtoto anaweza kusoma “nyumba” badala ya “nyumbani”. Tumia virai kama, “Tuitazame kila herufi, na tulijaribu neno hili tena.”
- Chagua Vitabu vya kusoma kuhusu matukio katika maisha ya mtoto wako, kama vile, kuanza shule, kwenda kwa daktari wa meno au kutunza wanyama, au kuhusu mada au shughuli ambazo anazipenda. Muunganishe na kusoma kwa kushirikisha kile matini yanachokufanya ufikirie.
- Mwambie na umhimize mtoto wako kuuliza maswali kuhusu matini mnayosoma. Unafikiri nini kitatokea baadae? Utabiri wako ulikuwa sahihi? Ni kwa namna gani hadithi ililingana na utabiri wako au ilitofautianaje? Mhusika huyu anajisikiaje? Ulisoma nini kilichokufanya ufikiri hivyo?
- Fanya mazoezi ya kuisimulia tena hadithi kwa kuuliza nini kilitokea mwanzoni, katikati na mwishoni. Simama baada ya kusoma kila sehemu, na upitie kilichotoke mpaka mlipo. Kwa kupitia “Clever App” ya mtoto wako, fika kwenye Maktaba ya Mtandaoni ya “Gale and KY” kwa makala za kuvutia.
- Wakati usomaji wa kimya ni stadi ya muhimu kwa mafanikio katika madarasa ya baadae, wanafunzi walio katika hatari ya kuto kufikia kiwango huhitaji muundo na msaada kutoka kwa wasaidizi wanaposoma kimya. Mtoto wako amewahi kusoma kwa sauti kabla ya kufanyia mazoezi kusoma kimya?
- Tembelea maktaba hizo wewe binafsi au kwa njia ya mtandao! Kwa taarifa kuhusu jinsi ya kupata maktaba ya umma karibu yako, tembelea ukurasa wa Maktaba ya Umma ya bure ya Louisville



- Elewa kwamba matini ni kitu chochote kinachowasilisha ujumbe. Mifano hujumuisha na si chini ya, vitabu visimuliavyo hadithi za kweli au za kubuni, mabango, nyimbo hotuba, kazi za sanaa, maelekezo kwa toi na ishara za barabarani.
- Nunua au tengeneza miche ya herufi (smaku, karatasi, plastiki) au mabo kwa mazoezi ya sauti
- Mwulize mwalimu wa mtoto wako khusu shughuli za EL za kufanya nyumbani kutoka Mtaala wa Elimu wa EL.

# MWONGOZO WA FAMILIA WA MPANGAO WASOMA NYUMBANI

## UTAMBUZI WA KIFONIMIKI NI NINI?

Utambuzi wa Kifonimiki ni uwezo wa kutofautisha, kuzalisha, kukumbuka na kung'amua sauti moja moja (fonimu) katika maneno yanayosemwa.

Stadi za utambuzi wa kifonimiki zinamtaka mtoto asikie na kucheza na sauti pasipo kusoma au kuandika, lakini huwezesha ukuzaji wa kusoma na kuandika. Shughuli zilizopo katika sehemu hii hazita jumuisha usomaji uandikaji maneno. Badala yake, mtoto wako atajikita katika sauti anazozisikia katika maneno ya kuongea na kufanya mazoezi ya kuyatamka maneno akizingatia sauti za mwanzoni, katikati na mwishoni mwa maneno. Kufanya mazoezi na sauti kwa dakika 5 – 10 kwa siku kunapendekezwa ili kutegemeza usomaji stadi.

Shughuli za utambuzi wa kifonimiki zilizomo kwenye mwongozo huu zimegawanyika katika vipengele viwili: shughuli za mwanzo na shughuli zenye changamoto zaidi ili kukuza stadi za mtoto wako katika yafuatayo:

- Kulinganisha sauti;
- Kuhesabu silabi;
- Kutambua sauti peke yake na zikiwa ndani ya maneno
- Kuongeza, kutoa na kubadilisha sauti katika maneno
- Kuvunja maneno katika sauti zake mbali mbali na kuyaunganisha tena; na
- Kuzitenga sauti.

## SHUGHULI ZA UTAMBUZI WA KIFONIMIKI

### Shughuli za Mwanzo:

Mwalimu wa mwanafunzi wako anaweza kuzirejea aina hizi za shughuli kama "shughuli za awali za utambuzi wa kifonolojia" kwa kuwa zinaweka msingi wa utambuzi wa kifonimiki. Shughuli hizi zinamruhusu mtoto wako kucheza na lugha (hujulikana pia kama mchezo wa maneno) ili kuvutia uzingativu wao kwenye lugha, sauti na silabi ndani ya maneno. Utaona mikwaju nyuma na mbele ya herufi katika sehemu hii, pamoja na baadhi ya sehemu za sauti. Unapoona hivi, tamka sauti ya herufi badala ya jina la herufi. Kwa mfano, unapoona /m/, tamka sauti ambayo huzalishwa na herufi "m" badala ya herufi "m". shughuli hizi zimepangwa kutoka nyepesi kwenda ngumu. Mwalimu wa mwanafunzi wako anaweza kupendekeza shughuli mahsusi, au unaweza kukamilisha shughuli kwa namna zilivyopangwa. Kurudia shughuli hizi kunapendekezwa.

**Kufanya mdundo**

- Eleza kwamba maneno yenye mdundo ni maneno ambayo huishia na sauti zinazofanana mwishoni. Toa baadhi ya mifano: sit/bit, bad/mad, sister/mister, kick/pick, chill/will.
- Mwambie mtoto wako aunde midundo. Mwulize, "Unaweza kuniambia neno lenye mdundo na cake?" (rake, sake, lake, fake). Maneno mengine ya kufanyia mazoezi: track, pail, man, skip.

**Kuzitambua Sauti Mwishoni mwa Maneno**

- Fikiria vitu au watu wa kuwaelezea. Mwambie mtoto wako akielezee kitu au mtu kwa neno linaloanza na sauti sawa na kitu au mtu.
  Mifano: "delicious donut," "bouncy ball," "green grass"

- Mwache mtotowako afikiri jina la kipuzi la familia au mrarfiki. Jina hilo jipya lazima angalau liwe na urefu wa maneno matatu na lazima lianze na sauti kama ya jina la mtu.
  Mifano: "handsome helpful Javier" au "creative character Kelly"

**Kuhesabu na Kucheza na Maneno, Sauti na Silabi**

- Mwambie mtoto wako kwamba mtafanya zamu kusema sentensi. Kwa kila neno kwenye sentensi, mchezaji mwingine atapata pointi moja. Fanyeni zamu kusema sentensi na kuhesabu maneno.
  Mfano: "She lives with her older sister and two dogs." (alama 9)
- Fanyeni mazoezi kuhesabu silabi za kwenye majina ya marafiki na wanafamilia.
  Mfano: Rob-ert (silabi 2), Ket-ur-ah (silabi 3), Lu-ci-a (silabi 3)
- Fanyeni mazoezi ya kuvunja maneno kuwa silabi. Baadhi ya waalimu huliita zoezi hili "kukunjua" neno, na mtoto wako anaweza kufanya huku anakunjua raba bendi. Tazama mtoto wako asiandike maneno na herufi za majina, bali sauti katika neno.
  Mifano: "Ni sauti gani huunda neno dog?" (/d/ /ŏ/ /g/) "Ni sauti gani huunda neno let?" (/l/ /ĕ/ /t/) "Ni sauti gani huunda neno kick?" (/k/ /ĭ/ /k/) "Ni sauti gani huunda neno shape?" (sh/ /ā/ /p/) "Ni sauti gani huunda neno drum?" (/d/ /r/ /ŭ/ /m/) "Ni sauti gani huunda neno snow? (/s/ /n/ /ō/)

## Shughuli Ngumu Zaidi:

Mwalimu wa mtoto wako anaweza kuzirejea aina hizi za shughuli kama "shughuli za utambuzi wa kifonimiki," au shughuli zinazowaruhusu watoto kufanya mazoezi ya kung'amua sauti mbalimbali katika maneno.

**Recognizing and Blending Sounds**

- Fanya mazoezi ya kusikia sauti moja moja katika maneno. Sema,
  "Sema neno hili baada ya mimi: Set." (Set) "Sauti ya kwanza ni nini?"
  (/s/) Sauti ya katikati ni nini?" (/e/) "Sauti ya mwisho ni nini?" (/t/)
  Maneno ya mazoezi na sauti 3: mat, tub, did, pot, sip, bed, kit
  Maneno ya mazoezi na sauti 4: stake, sled, Fred, plum, drip, flat
- Mpe mtoto wako sauti moja moja na umwambie aunganishe sauti hizo kuunda maneno Mifano: "Je, sauti /l//ĕ//g/ huunda neno gani?" (leg) "Je, sauti /c//r//ŏ/ /p/ huunda neno gani?" (crop) "Je, sauti /sh/ /ū/ huunda neno gani?" (shoe) "Je, sauti /m/ /ē/ huunda neno gani?" (me)

**Kubadilisha na Kufuta Sauti**

- Fanya mazoezi ya kubadilisha sauti za mwanzoni na mwishoni mwa maneno. Sema, "Hebu tuone kama tunaweza kuunda maneno mapya kwa kubadilisha sauti moja tu. Kama nikibadili /b/ katika bat kuwa /r/, ninapata neno gani jipya?" (rat)
  Examples: "Kama nikibadilisha /w/ katika wag kuwa /t/, ninapata neno gani jipya?" (tag) "Kama nikibadili /l/ katika shell kuwa /f/, Ninapata neno gani jipya?" (chef) "Kama nikibadili /p/ katika poodle kuwa /n/, ninapata neno gani jipya?" (noodle) "Kama nikibadili /tch/ katika witch kuwa /n/, ninapata neno gani jipya?" (win) "Kama nikibadili /s/ katika race kuwa /z/, ninapata neno gani jipya?" (rays)
- Fanya mazoezi ya kufuta sauti kwenye maneno.
  Mifano: "Sema potato bila /pō/." (tato) "Sema stop bila /s/." (top) "Sema peas bila /p/." (ease) "Sema sheet bila /t/." (she)

# MWONGOZO WA FAMILIA WA MPANGAO WASOMA NYUMBANI

## ELIMU YA SAUTI NI NINI?

Ni ujuzi wa uhusiano unaotabirika kati ya fonimu na herufi mwambatano (herufi au muunganiko wa herufi unaowasilisha fonimu) na uhusiano kati ya mafungu makubwa ya herufi na silabi au sehemu za maneno zenye maana (mofimu).

Madhumuni ya maelekezo ya elimu ya sauti ni kufundisha uhusiano baina ya herufi na sauti zinazounda ili kwamba wasomaji wawe na stadi wanazohitaji kusema maneno. Kusema maneno pia hujulikana kama **kutamka maneno**. Mtoto wako anapoweza kusema (au kutamka) maneno kwa haraka na kwa usahihi, huwa na stadi imara za elimu ya sauti.

Watoto hujenga stadi imara za elimu ya sauti kupitia maelekezo ya moja kwa moja na mazoezi. Stadi imara za elimu ya sauti huwaruhusu wanafunzi kutumia muda mwingi wakifikiri kuhusu kile ambacho maneno yanawaambia (maana zake) kuliko kugundua kile neno linachosema katika ukurasa.

Shughuli za elimu ya sauti katika mwongozo huu zitamsaidia mtoto wako kukuza uelewa wa stadi zinazoonyesha jinsi:

- Herufi zinavyowasilisha sauti;
- Uhusiano kati ya herufi na sauti zake ulivyo wa kutabirika;
- Wakati mwingine sauti moja tu huundwa na herufi mbili au zaidi zilizoungana;
- Maeneo yanayotabirika huamua sauti za irabu;
- Mara nyingi irabu mbili au moja hufanya kazi pamoja kuunda sauti moja ndefu au fupi;
- R inapoifuata irabu, huibadiri sauti ya irabu hiyo; na
- Maneno marefu huundawa na silabi fupi zaidi ambazo zinaweza kutamkwa sehemu moja baada ya nyingine


Mara nyingi, wanafunzi wanaopata shida na elimu ya sauti huhitaji mazoezi zaidi ya sauti. Ikihitajika, mrejee au mwombe mwalimu wa mwanafunzi wako akupe sehemu ya Utambuzi wa Kifonimiki ya mwongozo huu kwa shughuli zinazolenga kuelewa na kung'amua sauti.

## SHUGHULI ZA ELIMU YA SAUTI

Shuhuli hizi hupanda taratibu kutoka nyepesi kuelekea ngumu zaidi. Mwalimu wa mwanafunzi wako anaweza kupendekeza shughuli, au unaweza kukamilisha shughuli hizi kulingana na mpangilio uliopo. Kurudia shughuli kunahimizwa.

### Herufi Huwasilisha Sauti.

- Chagua herufi na mwache mtoto wako atafute vitu vitano vinavyoanza na sauti ya herufi hiyo. Kama sauti lengwa ni /m/ mtoto anaweza kupata mop, mat, mom, money, na microwave. Kila kitu kinapopatikana mwache mtoto wako afanye mazoezi ya kuiandika herufi m na kusema jina la kitu husika.
- Weka miche ya sumaku ya heruki kwenye friji. Taja majina ya herufi au sauti za herufi huku ukiandaa chakula, na mwache mtoto wako atoe miche inayofanana na sauti za herufi ulizotamka kutoka kwenye friji.
- Mwache mtoto wako atumie udongo wa michezo kusokota na kuunda maumbo ya herufi mbali mbali. Tamka majina ya au sauti za herufi hizo na umtazame akiunda maumbo ya herufi hizo.



# MWONGOZO WA FAMILIA WA MPANGAO WASOMA NYUMBANI

**Uhusiano Kati ya Herufi na Sauti Zeke Hutabirika.**

*Shughuli hizi hufanya mazoezi ya kusoma na kuandika maneno ya silabi moja kama bat, ham, sun au lip*

• Unda familia ya neno kwa kutumia herufi za sukamu upande kwa upande ili kuwasilisha sauti za katikati na mwisho za neno. Mwambie mtot wako kuzifikilia herufi moja moja ambazo zingeweza kuongezwa mwanzoni ili kuunda maneno. Mwache mtoto wako asome kwa sauti na kuandika neno wanaloliunda kabla ya kuunda neno jipya.

Mfano: Kama sehemu ya mwisho wa familia ya neno “op”, chagua sumaku o na p na herufi m ingeweza kuongezwa mwanzoni ili kuunda mop, na t ingeweza kuongezwa mwanzoni pia kuunda neno top. Maneno mengine ambay yangeweza kutengenezwa ni pop, cop, sop, lop. Hata maneno ya kubuni kama nop, rop na yop huwafurahisha watoto wakisoma na kuyaandika wanapofanyia mazoezi familia za maneno.

• Ukitumia moja kati ya orodha hapo chini, andika herufi zinazound maneno kwenye miraba midogo ya karatasi au karatasi za gundi. Kwa shughuli ya kwanza, andika herufi moja kwa kila mraba. Kwa shughuli ya pili, chagua herufi za mwanzo kutoka kwenye moja ya seti za herufi hapo chini ili uandike neno moja kwa kila mraba na kisha uandike herufi za mwishoni kutoka kwenye seti hiyo hiyo kwenye mraba mwingine. Msaidie mtoto wako aunde maneno kwa kutumia kadi za herufi ulizo ziunda. Kwa shughuli ya kwanza, zungusha kati ya kutoa herufi ya mwanzoni na ya mwishoni na kumwomba mtoto wako kutoa herufi ya katikati na kisha kutoa herufi ya katikati na kumwambia mtoto wako abuni mwanzo na mwisho ambao utaunda neno. Kwa shughuli ya pili, wakati mwingine toa mwanzo na mwambie mtoto akupe mwisho, na wakait mwingine toa mwisho na kumwambia mtoto wako atoe mwanzo.

Shughuli #1, Orodha #1: b, a, t, r, e, d, s, u, n, l, i, p, c, u (bat, red, sun, lip, cup, sit)
Orodha #2: t, i, p, l, e, r, u, n, o, b, c (tip, let, run, pin, rob, cop)
Orodha #3: s, e, t, n, l, p, r, i, h, a, m, o (set, nip, rip, ham, tan, pop)
Shughuli #2, Orodha #1: herufi za mwanzo – l, s, t; herufi za mwisho – op, it, et (sit, set, sop, lit, top)
Orodha #2: herufi za mwanzo – c, p, r; herufi za mwisho – at, up, un (pat, pun, cup, cat, run) List #3: herufi za mwanzo – c, d, t; herufi za mwisho – en, ot, an (den, ten, cot, dot, can)

Shughuli hizi hufanya mazoezi ya kusoma na kuandika maneno ya silabi moja yaliyo marefu zaidi kama clot, trim, slap, rust. Maneno haya yana herufi za mwanzo au za mwisho ambazo zinashikana pamoja, na sauti zote zinaweza kusikika. Baadhi ya mifano ya herufi hizi ni cl, tr, sl, na st. huitwa **miambatano**.

**Mara Nyingine, Sauti Moja Tu Huundwa na Herufi Mbili au Zaidi Zilizoambatana.**

*Mfano wa herufi ambazo hufanya sauti moja tu zinapoambatana pamoja hujumuisha sh, ch, th na tch. Hizi huitwa dayagrafu (herufi 2) na trayagrafu (Herufi 3).*




• Tumia chaki kuchora jedwari la taarifa la hopskochi. Katika kila kisanduku, andika herufi. Kwenye visanduku ambavyo vinakaa viwili kwa ulalo (mche-ulalo), andika herufi zilizopo kwenye orodha hapo chini. Mtoto anaporukia kwenye kisanduku mwambie ataje jina la herufi na sauti yake. Mtoto anaporukia mche-ulalo, mwambie aseme jina la herufi ya kisanduku cha kushoto, kisha rukia herufi ya kwenye kisanduku cha kulia na useme jina lake kabla hatimay ya kusema sauti ambayo herufi zote mbili huunda zinapoambatana.

Herufi za mifano kwa visanduku: b, d, f, j, k, m, p, r, s, t, w

Herufi za mfano kwa mche ulalo: ch, kn, ph, sh, th, wh, wr, ck

**Mara Nyingine Irabu Mbili Huunda Sauti Mpya.**

*Miunganiko ya irabu ambayo hufanya hivi huitwa diftonga (neno hili lina sauti "ph" /f/. zipo aina mbili ambazo ni maarufu sana katika lugha ya Kiingereza, nazo ni /oi/ kama kwenye coin au boil na /ou/ kama kwenye loud, au now. Mifano ya maneno mengine ambayo yana sauti hizi hujumuisha oil, toil, out na bout*

• Tumia notikadi au vipande mraba vya karatasi na seti za herufi zilizopendekezwa hapo chini kwa shughuli hii. Chagua seti ya herufi. Andika herufi kwenye kila notikadi tofauti ya kipande mraba cha karatasi. Weka kadi hizo katikati yako na mtoto. Kwa pamoja, someni harufi za kwenye kadi na mfanye mazoezi ya sauti kwenye kila kadi iliyoandikwa. Sasa, fanyeni zamu mkiunda maneno na herufi hizo. Mnaweza kuufanya mchezo kuona ni nani anaweza kuunda maneno mengi zaidi kutokana na herufi hizo. Kila neno lina pointi moja. Chezeni tena kwa kutumia seti mpya ya herufi.

Seti #1: ow, pr, c, n, fl, er (cow, now, flower, prow)
Seti #2: ou, nd, pr, cl, d, l, r, s, t, p (cloud, loud, proud, round)
Seti #3: oi, l, s, t, b, f (oil, soil, toil, boil, foil)

**R Inapoifuata Irabu, Huibadilisha Sauti ya Irabu Hiyo.**

*Hii pia huitwa miunganiko ya irabu-r au irabu zinazodhibitiwa na r. Mifano ya maneno ambayo yamebadilika sauti ya irabu kwa sababu ya herufi r hujumuisha maneno kama art, torn, march, car, sport, her, burn na first.*

• Tumia notikadi au vipande mraba vya karatasi na seti za herufi zilizopendekezwa hapo chini kwa shughuli hii. Chagua seti ya herufi. Andika herufi kwenye kila notikadi tofauti ya kipande mraba cha karatasi. Weka kadi hizo katikati yako na mtoto. Mwache mtoto wako achukue kadi moja badala ya nyingine toka kwenye bakuli mpaka ziishe. Kila anapochukua kadi mpya, wajaribu kuunda neno jipya kwa kadi walizo nazo. Wahimize waandike maneno mengi kadri inavyowezekana kwa kutumia herufi wanazozitoa bakulini. Hakikisha wanayasoma maneno wanayoyaunda na utazame jinsi irabu zinavyounda sauti tofauti kwa sababu ya kuwa karibu na herufi hiyo.

Seti #1: (maneno ya ar) c, ar, t, sh, ar, p, m, ar, k, f, ar, m
Seti #2: (maneno ya er) h, er, d, g, er, m, cl, er, k, p, er
Seti #3: (maneno ya ir) sh, ir, t, b, ir, d, c, ir, cle, f, ir, st, b, ir, th, day
Seti #4: (maneno ya or) sh, or, t, c, or, n, st, or, y, p, or, t
Seti #5: (maneno ya ur) h, ur, t, t, ur, tle, b, ur, n, p, ur, ple

**Maneno Marefu Zaidi Huundwa na Silabi Fupi Ambazo Zinaweza Kutamkwa Moja Baada ya Nyingine.**

*Kuandika na kusoma maneno yenye silabi zaidi ya moja hujumuisha maneno mwambatano na maneno yenye viambishi vya awali na tamati. Mifano ya maneno kama haya hujumuisha rainstorm, landing na retell.*

• Cheza michezo ya kuunda maneno kama vile Scrabble©, Boggle© au Word Up© na mtoto wako.

• Tumia vipande mraba vya karatasi (kuikata notikadi moja katika vipande mraba ni nzuri zaidi) kisha tumia seti ya silabi iliyopendekezwa hapo chini kwa shughuli hii. Andika silabi moja kwa kadi au kipande cha karatasi. Soma neno kutoka kwenye seti ya maneno uliyochagua na mwambie mtoto wako aunde neno kwa kutumia kadi za silabi. Anapochukua kila silabi, mwambie akusomee kadi hiyo. Mara wanapounda neno zima, mwambie mtoto aseme sehemu za neno kwa sauti na kisha asome neno zima. Zungumza kuhusu maana ya neno hilo na fanya mazoezi kwa kutumia neno hilo katika sentensi. Mpe changamoto ya kuunda maneno zaidi mtoto wako, akitumia sehemu za maneno ambazo bado hazijatumika.

Seti ya Silabi #1: (park, look, open, sing, watch, ing, re, un, ed, s, es)
parked/looking/parks/reopening/singing

Seti ya Silabi #2: (close, trust, heat, block, charge, dis, un, re, ing, s, ing)
disclose/closing/reheat/unblock/charges

Seti ya Silabi #3: (act, cover, draw, load, make, re, ing, tion, s, dis, un)
action/discover/drawing/unload/making

# MWONGOZO WA FAMILIA WA MPANGAO WASOMA NYUMBANI

## UTIRIRIFU NI NINI?

Utiririfu ni uwezo wa kusoma matini kwa kasi na usahihi wa kutosha ili kuwezesha ufahamu. Hii hujumuisha:

- Utambuzi wa maneno wa kiotomatiki;
- Utambuzi sahihi wa maneno;
- Use of expression when reading aloud matumizi ya ishara wakati wa kusoma kwa sauti; na
- Kuelewa kinachosomwa, kwa sauti na kimya kimya.

Utiririfu ni matokeo ya stadi imara za utambuzi wa kifonimiki na elimu ya sauti. Kama mwanafunzi anapata shida kusoma kwa kasi na kwa usahihi, anaweza kuhitaji mazoezi zaidi ya Utambuzi wa Kifonimiki na Elimu ya Sauti kutoka kwenye sehemu ya mwongozo huu. Ongea na mwalimu wa mtoto wako ili kuona ni ipi kati ya shughuli hapo chini inaweza kufaa zaidi.

Lengo kuu la mazoezi ya utiririfu mara zote ni kwa mtoto kuelewa anachokisoma. Mtoto anapoweza kusoma kwa utiririfu, anaweza kuzingatia kidogo zaidi kwnye kung'amua (kusoma) neno moja baada ya jingine na kuzingatia zaidi kwenya ujumbe wa jumla wa matini.

## SHUGHULI ZA UTIRIRIFU

*Shughuli hizi zimepangwa kwenye makundi matano ambayo yanaweza kuwezesha utiririfu. Mwalimu wa mtoto wako anaweza kupendekeza shughuli mahsusi, au unaweza kutimiza shughuli hizi kama zilivyopangwa. Kurudia shughuli kunahimizwa.*

**Kusikiliza Mifano ya Usomaji Tiririfu na Usomaji wa Ishara**

- Msomee mtoto wako kila siku! Unaposoma kwa sauti na mtoto wako wa umri wowote, unaonyesha kwa vitendo mfano wa namna usomaji tiririfu unavyokuwa.
- Tafuta fursa kwa mtoto wako ili aweze kusikiliza na kufuatisha rekodi za sauti. YouTube, StoryOnline na maktaba za ndani zina aina mbali mbali za hadithi zilizorekodiwa.
- Tumia ishara za kufaa unaposoma mahojiano. Kwa mfano, kama mhusika ana shauku ya kutembelea hifadhi, unaweza kuongea kwa sauti ya sahuku na umtie moyo mtoto wako kujumuisha hisia pia anaposoma.


**Chagua Vitabu kwa Kufanya Mazoezi ya Utiririfu.**

- Kila mara unaweza kufanya mazoezi ya utiririfu kwa kutumia vitabu ambavyo mwalimu wa mtoto wako anawatumia nyumbani na kuvipendekeza.
- Tumia kanuni ya "Vidole Kumi". Mwambie mtoto wako achague vitabu kutoka maktaba au vilivyoko nyumbani. Mwambie asome kurasa 2 – 3 kwa sauti. Kama mtoto wako akikosea neno 1 kati ya 10, kitabu hicho kinamfaa kwa kufanyia mazoezi utiririfu. Kama mtoto wako anakosea neno 1 kati ya 5, kitabu hicho kinakufaa wewe kusomakwa sauti, lakini kinaweza kuwa kigumu mno kwake.

**Someni Pamoja**

- Fanya mazoezi ya usomaji wa sauti ya juu na mtoto wako. Tumia hadithi au matini ngeni na usome vipande vidogo vya maneno (maneno 5 – 8) kwa kutumia kidole chako kutembeza pale unaposoma. Baada ya kumaliza mwache mtoto wako asome kwa sauti ya juu pia wa kile ulichosoma kwa kasi na ishara zile zile.
- Fanya mazoezi ya usomaji wa pamoja (au kusoma maneno pamoja kwa wakati mmoja). Unaweza kuonyesha mfano wa usomaji tiririfu na kumhimiza mtoto asome katika kiwango chako.
- Wasomee hadhira mbali mbali, pengine ukijumuisha majirani, babu na bibi, wanyama wa nyumbani, midoli au wanafamilia wachanga. Msomaji anapowaweka hadhira kichwani, hujua namna ya kuwa watiririfu na wenye kutumia ishara.

# MWONGOZO WA FAMILIA WA MPANGAO WASOMA NYUMBANI





### Usomaji wa Kurudiarudia na Kukata Kiasi cha Maneno

- Soma hadithi moja mara nyingi. Usomaji wa kurudia wa hadithi humsaidia mtoto kuwa na utambuzi wa maneno na sauti wanazoziunda wanaposoma kwa utiririfu.
- Soma sentensi au vifungu pendwa na mtoto wako. Soma vifungu kwa sauti, na halafu someni pamoja kwa pamoja kwa wakati mmoja, ukimsaidia mtoto wako ang'amue maneno aliyoyakosea, ukimweleza makosa yoyote anayoyafanya. Kisha, mwache mtoto akusomee kifungu akizingatia usahihi. Hatimaye, mwache mtoto akusomee kifungu tena, akizingatia utiririfu na ishara. Lengo ni kusikika mwororo na kawaida.
- Rekodi usomaji. Baada ya mtoto wako kufanyia mazoezi kifungu, rekodi usomaji kwa kutumia simu ya mkononi au kifaa kingine cha kurekodi. Mtoto wako anaweza kusikiliza usomaji wake na kufuatisha kwnye kitabu. Unaweza kurudia hatua hii mkiwa pamoja kuhakikisha kila rekodi inakuwa bora zaidi kila mara.
- Kwa kutumia penseli, chora mistari kati ya maneno unaposikia pumziko la kawaida. Mfanye mtoto afanyie mazoezi usomaji wa kifungu kizima, akiunganisha maneno kati ya mistari ya penseli anaposoma.

  Mfano: "Tangu wakati huo, / kil mchana, mapema mara mama yake / alipoondoka kwa ajili ya bingo, / Matilda angetambaa / kuelekea maktaba. // Kutembea kulimchukua / dakika kumi tu/ na hii ilimruhusu / masaa mwaili mazuri/ akiketi kimya / peke yake / kwenye kona tulivu / akimeza kitabu kimoja baada ya kingine." (kutoka Matilda by Roald Dahl)

### Kusoma kwa Ajili ya Kasi

- **Kwa watoto ambao wametoka tu kujifunza sauti za herufi**: Fanya mazoezi ya kusema majina ya herufi haraka kutoka kwenye orodha ya herufi kubwa na ndogo. Sema "Hebu tuone ni herufi ngapi unaweza kuzitaja kwa dakika moja". Ili kulifanya hili lionekane kama mchezo kuliko zoezi, mpe changamoto mtoto ya kusoma herufi zaidi kwa kila jaribio.

  Orodha ya mfano: H o j L s W t g R p Q a A c x D O

- **Kwa watoto wajifunzao maneno picha kwa darasa lolote:** Utambuzi wa maneno wa kiotomatiki huwezesha usomaji tiririfu. Unaweza kufanya mazoezi ya kusoma maneno kutoka kwenye orodha iliyotolewa na shule ya mtoto wako na ujaribu kuisoma haraka kila mara. Kuyaweka maneno kwenye flashikadi ili kucheza michezo ya kumbukumbu na kuoanisha kunaweza pia kuwezesha utambuzi wa kiotomatiki wa maneno.

# MWONGOZO WA FAMILIA WA MPANGAO WASOMA NYUMBANI

## MSAMIATI NI NINI?

Msamiati ni ujuzi wa maneno moja moja na maana zake kwenye matini na dhana ambazo maneno yanawasilisha. Hii hujumuisha:
- Kuelewa maneno wakati wa kusoma au kusikiliza, na
- Kutumia maneno wakati wa kuandika au kuongea.

Baadhi ya watafiti wanabashiri kwamba mtoto wa wastani anayeingia shule ya awali hujua takribani maneno mapya 4,000 na atajifunza maneno 800 mpaka 1,000 kila mwaka mpaka darasa la 6. Watafiti wengine wanakadiria kwamba watoto wanaweza kujifunza maneno mapya 2,000 mpaka 3,000 kila mwaka! Watoto wanaweza kujifunza maneno mapya kwa mfululizo wakiwa nyumbani na shuleni, hasa wa wakiyatumia sana maneno mapya.

**Ujumbe kwa familia za lugha mbili na lugha nyingi:**
**Kuzungumza lugha nyingi ni kipawa! Ungiongea lugha nyingine mbali na Kiingereza nyumbani, ukimfundisha mtoto wako maneno mengi kwa lugha yako ya nyumbani itaimarisha pia ujuzi wao wa misamiati ya Kiingereza. Msamiati mkubwa kwenye lugha ya/za nyumbani ya/za mtoto wako itapelekea ukuaji wa msamiati kwenye Kiingereza.**

## SHUGHULI ZA MSAMIATI

**Kutumia Mazungumzo Kujenga Msamiati**

- Uliza maswali ya wazi, au maswali ambayo hayana jibu la neno moja. Maswali ya wazi humhimiza mtoto wako kufikiri yeye mwenyewe na kukua katika kueleza mawazo yao.

  Mifano: Nini kilikufurahisha katika sehemu yetu ya siku? Kwa nini? Nini kinakufanya ufurahie ____? (ingiza mchezo, shughuli, onyesho, chakula au sehemu) Unafikiri nini kitatokea kama …? Unafikiri tufanye nini ...?
- Uwe na mazungumzo na mtoto wako wakati wa chakula cha jioni au wakati mkiendesha gari. Ongea sana kadiri iwezekanavyo kuhusu kile unachokiona, popote mlipo. Kuongea kuhusu siku ya mtoto wako shuleni, mipango ya wikendi au kumbukumbu zinazofahamika kunaweza kukuza msamiati wa mtoto wako.

**Kutumia Uzoefu wa Maisha Kujenga Msamiati**

- Tengeneza fasiri rafiki kwa mtoto kwa maneno unayoyaona na kusikia. Kwa mfano: “Neno bonge humaanisha kitu fulani kikubwa kweli, kweli”. Kisha, tumia neno hilo kwenye maisha yako ya kila siku. “Aaah! Tazama wingu lile! Ni bonge la wingu”!
- Unapoona kitu au alama ya ardhi nyumbani au kwenye ujirani wenu, ona ni kiasi gani cha maneno unaweza kuunda kuhusiana na kitu au alama hiyo ya ardhini. Sema, “Hebu tuone ni kiasi gani cha maneno tunaweza kupata ambayo yanajirudia kwa njia ya reli?” (Njia za reli, matreni, kukutana, magari, honi, magurudumu, lilisimama, taa, tingo, injini, kabuzi)
- Cheza na homonimia, au maneno ambayo yana sauti sawa lakini maana zake ni tofauti. Sema, “Tazama mti huu. Tunauitaje mti ulioko nje ya mti?” (bark) “Bark inaweza kuwa na maana gani zaidi?” (Sauti aifanyayo mbwa).

  Homonimia nyingine za kufanyia mazoezi: • Ring (kipande cha kito na mlio ya simu au kengele ya mlango) • Flu/flew (ugonjwa au tensi ya wakati uliopita ya fly) • Pain/pane (maumivu au kioo dirishani)

# MWONGOZO WA FAMILIA WA MPANGAO WASOMA NYUMBANI

**Kutumia Matini Kujenga Msamiati**

- Someni matini za taarifa (zisizo za kubuni) pamoja kujifunza kuhusu mada zinazohusiana na maslahi ya mtoto wako. Ongea kuhusu maneno baada ya kusoma na yaonyeshe kwenye maisha yako ya kila siku.
- Kabla ya kusoma kitabu kwa sauti, tambulisha maneno yoyote mapya yenye changamoto. Eleza maana ya maneno na mwambie mtoto wako aliseme kila neno. Huku ukisoma, onyesha maneno na kueleza maana yake tena.
- Soma ishara za barabarani, mabango na alama nyingine kwa sauti kwa mtoto wako. Ongea kuhusu maana ya maneno hayo.
- Tazama filamu na vipindi pendwa vya televisheni pamoja na mtoto wako ukizingatia katika kusikiliza maneno makuu ya kuanza kuyatumia nyumbani. Yatumie maneno haya kwenye mazungumzo yako ya kila siku.

**Kujifunza Sehemu za Maneno Kujenga Msamiati**

*Shughuli hizi ni za juu zaidi. Watoto wanaoelewa jinsi sehemu za maneno zinavyoungana pamoja ili kubadilisha maana za maneno wanaweza kusoma na kutambua maana za maneno mapya.*

Kazia kile mtoto wako anachokisoma kuhusu viambishi vya awali na viambishi tamati shuleni. Viambishi vya Awali ni sehemu za maneno ambazo zinaweza kuongezwa mwanzoni mwa neno kubadili maana yake. Viambishi Tamati ni sehemu za maneno zinazoweza kuongezwa mwishoni kubadili maana yake.

| Viambishi vya Awali vya Mazoezi | Viambishi Tamati vya Mazoezi |
|---|---|
| **dis- (si, hakuna, kutokuwepo kwa) pre- (kabla) re- (tena, nyuma)** | **-s/es (zaidi ya kimoja) -ed (wakati uliopita wa matendo) -tion (hali ya)** |




- Onyesha maneno yenye viambishi vya awali unaposoma vitabu au unapoviona kwenye ishara au matangazo. Zungumza kuhusu jinsi maana za maneno zinavyobadilika unappongeza viambishi awali na tamati.
- Anza na mzizi au neno kama act. Fanya kazi na mtoto wako kuandika maneno mengi iwezekanavyo ambayo yanatumia neno hilo na kujadili jinsi kiambishi hiki cha awali kinavyobadilisha maana za maneno. Kutokana na act, react, reacted, reacting, na reaction. Maneno mengine ya kujaribu ni flect, heat au inform.

# MWONGOZO WA FAMILIA WA MPANGAO WASOMA NYUMBANI

## UFAHAMU NI NINI?

Mchakato tata wa kuelewa na kutia mantiki kwenye matini iliyoandikwa kwa njia ya kung'amua, ujuzi wa awali na kufikiri kwa sauti, ambapo vyote hutumiwa na wasomaji wazuri kuelewa, kukumbuka na kuwasilisha kile kilichosomwa

Ufahamu huwataka wanafunzi, si tu kuwa na utambuzi wa kifonimiki imara, elimu ya sauti, utiririfu na stadi za msamiati, bali pia huwataka wanafunzi kutumia ujuzi wa awali, ujuzi wa miundo ya sentensi, uwezo wa kudhania (kuvuta mahitimisho mapya) na ujuzi wa matini mbali mbali.

**Ufahamu ndilo lengo kuu la usomaji.** Kuzimudu stadi zote hizo ni muhimu kwa sababu huwaruhusu watoto wazingatie ufikiriaji makini na kuchakata uelewa unaohitajika ili kuelewa na kuchambua kile wanachokisoma.

Watoto wenye ufahamu mkubwa wa usomaji:
- Huchunga uelewa wao binafsi na kusoma tena au kujadili matini endapo haileti maana;
- Hujua lengo lao la kusoma (kujifunza taarifa mpya, ili kushawishika au kuburudika);
- Hudhania (kuvuta mahitimisho mapya) kutoka kwenye matini;
- Huweka taarifa kwenye mpangilio akilini mwao wanaposoma; na
- Huelewa jinsi taarifa mpya inavyohusiana au kubadili ujuzi wao na imani zao za sasa.

## SHUGHULI ZA UFAHAMU

### TipsVidokezo vya Jumla vya Ufahamu

Soma matini za taarifa na fasihi. **Matini za taarifa** ni zile zisizo za kubuni na hutokana na ukweli, matukio na watu wa kweli. Matini za taarifa zinaweza kujumuisha wasifu wa watu, maelezo ya kihistoria, maelezo ya kisayansi, chati na grafu za kihisabati na vingine. **Fasihi au matini za fasihi** wakati mwingine huitwa za kubuni na huhusisha matukio na watu wa kufikirika. Matini hivi zinaweza kujumuisha ushairi, maigizo, hadithi fupi, ngano na novela.

- Zungumza kuhusu mizunguko mtakayofanya pamoja. Tumia maneno ya hatua (kwanza, halfu, mwisho, hatimaye) unapoelezea siku yako. Kwa mfano, unaweza kusema, "Tutakuwa na vituo vitatu. Kwanza, tutakwenda kwenye kituo cha mafuta, Halafu, tutakwenda benki. Hatimaye, tutakwenda kwenye duka la mahitaji madogo."
- Hadithi ambazo watoto huzifurahia zipo kila mahala kwenye vyombo vya habari huzifurahia zaidi ya vitabu vilivyochapwa. Jadili kuhusu filamu, vidio, vidio ya mchezo wa kompyuta au kipindi cha televisheni: "Nani walikuwa wahusika wakuu/washiriki? Walikuwa na matatizo ya aina gani? Walijaribu kutatua matatizo hayo kwa njia gani? Filamu ilianzaje? Kipindi kiliishaje?

### Shughuli za KABLA ya Usomaji:

- Mwache mtoto wako asome kichwa cha kitabu na kwenda ukurasa kwa ukurasa akipitia matini ya kitabu. Mwulize anafikiri hadithi itahusu nini. **Namna nyingine**: Kama unasoma matini ya taarifa, mwache mtoto wako atazame vipengele mbali mbali vya matini (vichwa vya habari, picha au taarifa za chini ya picha) ili vimsaidie kufanya ubashiri kuhusu matini.
- Zungumza na mtoto wako kuhusu kile ambacho tayari anakifahamu kuhusu mada au wazo. Mwambie kile mtoto wako anachoweza kujifunza au anachotaka kujifunza kutokana na kusoma kitabu hicho. Mchakato huu huitwa **kuandaa kusudi** na unaweza kuongoza ufahamu.
- Kama unasoma kitabu chenye sura kwa siku kadhaa, mwache mtoto wako ajimumbushe kabla ya kuanza sura mpya. Sema, "Fikiri nyuma tulikosoma mara ya mwisho. Wahusika walikuwa nani? Walikuwa wanajaribu kukamilisha nini? Taarifa kutoka kwenye hadithi zilituambia nini kuwahusu?" Kusoma kuanzia kwenye ukurasa uliosomwa mara ya mwisho unaweza kuwa wa muhimu.

# MWONGOZO WA FAMILIA WA MPANGAO WASOMA NYUMBANI

## Shughuli za WAKATI Usomaji:

- Unapomsome mtoto wako kwa sauti, zungumza kuhusu kile unachofikiri. Hii ni fulsa ya kumwonyesha mtoto wako kwamba kuna kikubwa zaidi katika usomaji kuliko kugundua maneno tu. Elezea kile unachofikiri kuhusu kinachoendelea kwenye kitabu au kile ulichofikiri kuhusu chaguo la mhusika.

  Simama kila baada ya kurasa kadhaa ili kukagua uelewa wa mtoto wako wa kile kinachosomwa. Uliza maswali ya nani, nini, lini, kwa nini na kwa jinsi gani. Kama mtoto wako hajui, rudi nyuma na usome tena ukionyesha kwamba wasomaji wakubwa husoma tena ikiwa hawaelewi kitu fulani.
- Msaidie mtoto wako jinsi ya kudhania maana kutoka kewnye kile ambacho hakijasemwa kwenye matini. Mhusika anapokuwa na tukio kubwa, mwambie mtoto wako afikiri jinsi mhusika huyo atakavyojihisi, au nini atafanya baada ya hapo kulingana na kile mhusika ameshafanya katika hadithi.
- Onyesha lugha ya kawaida na ile ya picha kwenye matini. Kawaida humaanisha matini husema hasa kile inachomaanisha, wakati lugha ya picha inaweza kukuza au kulinganisha. Kwa mfano, “Kitabu kinasema kwamba begi la mgongoni la Maria lina uzani wa tani moja. Unadhani matini inamaana hiyo? Kwa nini au kwa nini hapana?”
- Mhimize mtoto wako awafikirie wahusika, eneo la tukio au matukio kutoka kwenye kitabu anachosoma. Mwambie mtoto aelezee, kwa kutumia taarifa za kwenye matini, nini anachokifikiria anaposoma.




## Shughuli za Baada ya Usomaji:

Mwambie mtoto wako akwambie nini kilitokea. Mwambie mtoto ajumuishe taarifa kuhusu mhusika mkuu, eneo na matukio makuu. Mhimize asimulie tena hadithi katika mtiririko sahihi wa matukio.

- Rudi kwenye lengo lako la usomaji: “Umejifunza kile ulichokusudia kujifunza?” Kama sivyo, fanya aina fulani ya utafiti mtandaoni au kwenye maktaba kujifunza zaidi.
- Baada ya kusoma, muulize mwambie mtoto wako **atengeneze mazo** lake kuhusu baadhi ya sehemu za matini na kutoa sababu kutoka kwenye matini ili kusimamia mawazo yake, “Unakubaliana na chaguo la mhusika? Nionyeshe sehemu hiyo. Kwa nini unakubali?”

  Uliza maswali kuhusu **tabia za wahusika, hamasa, vitendo au hisia**. “Unadhani ni mhusika gani alikuwa mkarimu? Ni mhusika gani alikuwa na majivuno? Ni matini gani kwenye kitabu yanatuonyesha hivyo?” Kama mtoto wako hajui, soma tena sehemu inayoonyesha jibu lako.
- Himiza ufikiriaji wa kimlolongo kwa kuuliza, “Kama hadithi ingeendelea, **unadhani nini kingetokea** mbele? Nini katika hadithi hii kinakufanya ufikiri hivyo? Ni kwa namna gani tukio kama hilo lingewaathili wahusika?”
- Msaidie mtoto wako **aunganishe mambo** na uzoefu au imani zake mwenyewe. Sema “Kuna chochote unachosoma kwenye hadithi kinachokukumbusha kuhusu kitu fulani kutoka maishani mwetu?”